



**SWAHILI A1 – STANDARD LEVEL – PAPER 2**  
**SWAHILI A1 – NIVEAU MOYEN – ÉPREUVE 2**  
**SWAHILI A1 – NIVEL MEDIO – PRUEBA 2**

Friday 6 May 2005 (morning)

Vendredi 6 mai 2005 (matin)

Viernes 6 de mayo de 2005 (mañana)

1 hour 30 minutes / 1 heure 30 minutes / 1 hora 30 minutos

---

**INSTRUCTIONS TO CANDIDATES**

- Do not open this examination paper until instructed to do so.
- Answer one essay question only. You must base your answer on at least two of the Part 3 works you have studied. You may include in your answer a discussion of a Part 2 work of the same genre if relevant. Answers which are not based on a discussion of at least two Part 3 works will not score high marks.

**INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS**

- N'ouvrez pas cette épreuve avant d'y être autorisé(e).
- Traitez un seul sujet de composition. Vous devez baser votre réponse sur au moins deux des œuvres de la 3<sup>e</sup> partie que vous avez étudiées. Le cas échéant, vous pouvez inclure dans votre réponse une discussion sur une œuvre du même genre littéraire étudiée dans la 2<sup>e</sup> partie du programme. Les réponses qui ne sont pas basées sur au moins deux des œuvres de la 3<sup>e</sup> partie n'obtiendront pas une note élevée.

**INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS**

- No abra esta prueba hasta que se lo autoricen.
- Elija un tema de redacción. Su respuesta deberá basarse en al menos dos de las obras estudiadas en la Parte 3. Se podrán hacer comentarios sobre una obra de la Parte 2 del mismo género, si fuera necesario. Las respuestas que no incluyan una discusión sobre al menos dos obras de la Parte 3 no recibirán notas altas.

*Jibu suala moja tu la insha. Jibu lako liegemee kwenye angalau kazi mbili za kazi za sehemu ya 3 ulizojifunza. Unaweza kuingiza katika jibu lako majadiliano ya kazi ya sehemu ya 2 ya utanze huohuo ambao umejitayarisha nao. Majibu ambayo **hayana** mjadala wa angalau kazi mbili za sehemu ya 3 **hayatapewa** alama nyingi.*

### **Tamthilia**

#### **1. Ama**

- (a) Kwa kulinganisha kazi mbili ulizojitayarisha nazo katika sehemu hii, onyesha VIPI kipengele cha “mazungumzo” kinavyotumika katika kazi hizo.

*Au*

- (b) “Migogoro ya tamthilia lazima itatuliwe hatimaye.” Jadili jinsi usemi huu unavyojitokeza katika kazi angalau mbili ulizojitayarisha nazo katika sehemu hii.

### **Riwaya**

#### **2. Ama**

- (a) Kwa kutumia kazi mbili ulizojitayarisha nazo katika sehemu hii, elezea VIPI waandishi wanajenga wahusika wao wakuu kulingana na maudhui ya kazi zao.

*Au*

- (b) Elezea jinsi “mitazamo ya msimulizi” inavyojitokeza katika angalau kazi mbili ulizojitayarisha nazo katika sehemu hii.

### **Ushairi**

#### **3. Ama**

- (a) Kwa kutumia angalau mashairi mawili katika diwani mbili za mashairi ulizojitayarisha nazo, jadili kipengele cha “arudhi” na umuhimu wake katika shairi la Kiswahili.

*Au*

- (b) Kwa kutumia mashairi ya washairi wawili uliojitarisha nayo katika sehemu hii, onyesha VIPI washairi hao wanavyojenga falsafa yao ya maisha kutokana na mambo wanayozungumzia.

## Riwaya ya Mapenzi

### 4. *Ama*

- (a) Jadili vipi mwanamke, kulingana na mwanamme, anavyotazamwa na waandishi wawili ambao kazi zao umejitayarisha nazo katika sehemu hii.

*Au*

- (b) “Riwaya ya mapenzi mara nyingi hujaa “chuku” au “vitiachumvi.” Ijadili kauli hii, huku ukitoa mifano kutoka angalau kazi mbili ulizojitayarisha nazo katika sehemu hii.

## Masuala ya Ujumla

### 5. *Ama*

- (a) “Kazi ya fasihi lazima iwe yenyе kusadikisha wasomaji.” Ijadili kauli hii kwa kuitolea mifano kutokana na angalau kazi mbili ulizojitayarisha nazo.

*Au*

- (b) Kwa kutumia kazi mbili ulizojitayarisha nazo, tofautisha waandishi wawili kuhusu nipi wanatumia mazingira katika kazi zao. Elezea yupi amekuvutia zaidi na kwa nini.

*Au*

- (c) “Kuchunguza na kufichua siri za maisha ni wajibu wa kila mwandishi wa kazi ya fasihi.” Ijadili kauli hii huku ukizingatia kazi za waandishi wawili ulizojitayarisha nazo.

*Au*

- (d) “Maudhui ya kazi za fasihi huweza kuathiriwa na matukio mbalimbali ya wakati fulani katika jamii husika.” Ijadili kauli hii kwa kuitolea mifano kutokana na kazi ulizojitayarisha nazo.